# VIPINDI SITA VYA MAISHA YA MWANADAMU

Jifunze kisha ujipime upo kwenye kipindi gani kati ya vipindi hivyo?

**1. Miaka 0-15 kuishi kwa maono ya mzazi.**

• Hapa mtoto anategemea kila kitu kutoka kwa mzazi

• Mzazi ndiye anayebeba maono kwa niaba ya mtoto wake

• Mzazi ndiye anayejua mtoto atakula nini, atavaa nini, asome au asisome shule, na afya ya mtoto kwa ujumla iko mikononi mwake

• Anachokiamua mzazi ndicho mtoto anafuata kwamba anapenda au hapendi.

Hiki ni kipindi ambacho mzazi awe makini sana na familia yake. Achague mambo mazuri na tija kupandikiza kwa mtoto wake.

Mtoto hapa ataiga kila kitu kutoka kwa wazazi kwa kuwatazama wanavyoishi na kujaribu kuiga yote yanayoyafanywa. Ni vema wazazi kuwa makini na aina ya mambo tunayoweza kuathiri ubongo wa mtoto yawe na faida kwa familia na taifa. Ukizoelea ulevi, ugomvi na kutofanya kazi (uvivu), mtoto atajua ndio staili ya maisha na yeye ataanza kufanya kama wewe. Mtoto atengenezewe mazingira ya kutimiza ndoto zake. Ashawishike na mambo makubwa ambayo familia yake inafanya. Mambo yasiyofaa yasifanywe mbele ya watoto. Jifunze kufanya kazi kwa bidii na kumtegemea Mungu pia uwafundishe watoto wako wajue kila unachopata ni kufanya kazi na kumtanguliza Mungu. Wazazi wengi wameshiriki kuharibu maono ya watoto wao. Kuna wazazi anaweza kukaa miezi yote mitatu na zaidi nje ya familia hajui alionana lini na watoto wake. Anaondoka asubuhi watoto wakiwa wamelala anarudi usiku watoto wakiwa wamelala. Anayejua habari ya baba ni mama tu. Baadaye watoto wanaondoa hisia ya baba kichwani na kwasababu wamama wengi hawapendi kuwakwaza watoto nyumbani kunatokea ugomvi kwamba watoto hawamuheshimu mama kwa sababu thamani ya mama ni kubwa sana anapokuwepo baba hasa katika malezi ya watoto.

Kwa utafiti inaonesha kuwa mtoto akifundishwa vizuri hata akijaribu kupoteza mwelekeo hasa kwasababu ya mabadiliko ya maumbile lakini roho na akili ya umakini wa mambo

aliyojifunza unabaki palepale hata akiyumba uwezo wa kusimama na kuendelea na safari ya kimaisha yenye ushindi nikubwa. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo; wanasema mtaani. Mtoto kwake kujua jambo jema na baya ni ngumu. Mzazi ndio kiongozi wa mtoto katika kutambua mambo mema na mabaya. Unapokuwa mtu mzima Roho mtakatifu anakuonya kuhusu jema na baya. Kwa mtoto haiko hivyo ila Roho wa Bwana ni wa kutosha kwa mzazi ili kutoa malezi bora yatakayo mletea mwanaye ushindi akiwa mtu mzima. MARKO 10:13-16.

**2. Miaka 15-25-kupata maono (dreaming season)**

Hapa ndipo safari ya maono ya mtu hutungwa (kuzaliwa), Nataka nije niwe mtu wa aina hii, Nataka baadaye nikimaliza masomo niwe fulani, Nikija kuoa/kuolewa nitakuja kuoa/kuolewa na mtu aina fulani, n.k Kipindi hiki kikipita utababaika sana kwenye vipindi vya mbele unaweza ukawa umekosea muda (timing) yako na kuivuruga ramani yako ya mbele ya maisha. Kijana unashauriwa kupanga mambo yako mapema kuhusu maisha yako ya baadaye. Utengeneze ramani ya maisha yako ya baadaye.

Hapa chini ni baadhi ya maswali ambayo waweza kujiuliza;

i. Unataka uwe nani?
ii. Unataka kuwa na mke /mume wa aina gani?
iii. Unataka ujenge nyumba ya namna gani?
iv. Unataka uishi maisha ya kiumaskini au kiutajiri?
v. Unataka ufikie kiwango gani cha elimu?
vi. Utafanya harusi ya namna gani?
vii. Unataka uwe na marafiki wa namna gani?
viii. viii. Unampango wa kusafiri ndani ya nchi yako na nje ya nchi yako?
ix. Unataka ufanye biashara ya namna gani?
x. Je unataka uwe na kampuni?
xi. Je unataka uwe muhubiri wa namna gani?

Usipokuwa na ramani kama hiyo itakayokuongoza kufanikiwa kimaisha hauwezi kutimiza jambo lolote katika maisha yako, zaidi utaishia kuwa fwata upepo. Nakuombea Kwa Mungu akupe akili na maarifa ya kuhuishwa tena ufanye jambo la

maana ukiwa hapa duniani kabla haujafa uache historia na urithi kwa familia na taifa. Maswali haya yanaweza kukufanya uwe na mandalizi sahihi kwa habari ya maisha yako ya baadaye (PREPARATIONS). MITHALI 29:18, HABAKUKI 2:2, 1YOHANA 2:14